

Masomo maalumu yahusuyo (Wanawake na mabinti).

Alamothi ni nini? Na nini ufunuo wake? (*1Nyakati 15:20*)

Jibu: Tusome,

1Nyakati 15:19 “Hivyo hao waimbaji, Hemani, Asafu, na Ethani, wakaagizwa kupiga matoazi yao ya shaba kwa sauti kuu;

20 na Zekaria, na Yaasieli na Shemiramothi, na Yehieli, na Uni, na Eliabu, na Maaseya, na Benaya, wenye vinanda vya SAUTI YA ALAMOTHI”

“**Alamothi**” maana yake ni “**wanawake vijana**”... Hivyo hapo anaposema vinanda vya sauti ya Alamothi, maana yake ni vinanda vya sauti za “**wanawake vijana**”.

Hiki ni kipindi ambacho Mfalme Daudi alikuwa analitoa sanduku la Agano la Bwana kutoka nyumbani kwa Ben-edomu na kulipandisha

Yerusalem.

Na wakati wanlipandisha Daudi aliwaanda wana wa Asafu (watu walio hodari wa kuimba) wenye matoazi pamoja na kundi lingine la watu *nane* (8) viongozi wa sifa, wenye vinanda vitakavyotoa sauti kuwafuatiliza wanawake vijana waimbaji (**Alamothi**).

Ni nini tunajifunza?

Kikubwa tunachoweza kujifunza ni jinsi "**wanawake walivyo na nafasi kubwa katika kumwimbia Mungu**". Daudi aliona, wana wa Asafu pekee haitoshi (ambao ni wanaume)zinahitajika pia *sauti za wanawake vijana*, katika kumwimbia Mungu. Na utaona jambo hilo Mungu alilikubali sana na likawa Baraka sana kwa Mfalme Daudi.

Na Mungu ni yule yule hajabadilika, kama alizikubali sifa za Daudi na kundi lake, atafanya hivyo hata leo, ikiwa tutasimama vyema katika nafasi zetu.

Ikiwa wewe ni mwanamke au binti.. fahamu kuwa sauti yako ni ya thamani sana katika kumwimbia Mungu, (*ndio maana si nzito kama ya mwanaume*). Hivyo chukua nafasi hiyo katika kulitimiza kusudi la Mungu ndani yako. Tafuta namna yoyote umwimbie Mungu na Bwana

atakubariki.

Zaburi ya 46 ambayo iliandikwa na wana wa Kora, ni Zaburi maalumu kwa ALAMOTHI. Ni nyimbo iliyokusudiwa iimbwe na Maalamothi, yenye kumtukuza Mungu kuhubiri uweza wake.

Zaburi 46:1 “Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso.

2 Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi, Ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari.

3 Maji yake yajapovuma na kuumuka, Ijapopepesuka milima kwa kiburi chake.

4 Kuna mto, vijito vyake vyaufurahisha mji wa Mungu, Patakatifu pa maskani zake Aliye juu.

5 Mungu yu katikati yake hautatetemeshwa; Mungu atausaidia asubuhi na mapema.

6 Mataifa yalighadhibika, falme zikataharuki; Alitoa sauti yake, nchi ikayeyuka.

7 *Bwana wa majeshi yu pamoja nasi, Mungu wa Yakobo ni ngome yetu.*

8 *Njoni myatazame matendo ya Bwana, Jinsi alivyofanya ukiwa katika nchi.*

9 *Avikomesha vita hata mwisho wa dunia; Avunja uta, akata mkuki, achoma moto magari.*

10 *Acheni, mjue ya kuwa Mimi ni Mungu, Nitakuzwa katika mataifa, nitakuzwa katika nchi.*

11 *Bwana wa majeshi yu pamoja nasi, Mungu wa Yakobo ni ngome yetu”*

Bwana akubariki.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link

hii >> <https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx>

JE WEWE NI ALAMOTHI?..BASI TIMIZA YAFUATAYO!

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

Mafundisho mengine:

**NAMNA YA KUITAMBUA SAUTI YA MUNGU INAPOZUNGUMZA
NA WEWE**

Kwanini wajane vijana hawakupaswa kuandikwa?

Ninyi mnaoimba nyimbo za upuzi pamoja na sauti ya vinanda.

TATIZO LA NDANI LINALOWASUMBUA VIJANA, WALIOOKOKA.

**Kuna watatu wenyе mwendo wa kupendeza Naam, wanne walio na
mwendo mzuri.**

Rudi nyumbani

Share on:

JE WEWE NI ALAMOTHI?..BASI TIMIZA YAFUATAYO!

WhatsApp